**NOA BONGO, JENGA MAISHA YAKO**

**"KABUMBU BARANI AFRIKA - NI ZAIDI YA MCHEZO!"**

**EPISODE SIX: "Timu Bora"**

**MUANDISHI: Chrispin Mwakideu**

**WAHARIRI: Andrea Schmidt, Thelma Mwadzaya**

**Orodha ya Washiriki/ KIPINDI CHA SITA:**

- Msimulizi

**SCENEONE: TAMBARARE CITY,CENTRAL BUSINESS DISTRICT**

- Mheshimiwa Makemba (mume, 55)
- Komora (Mume, 14)

**SCENE TWO: AUNT LILY WAKES UP**

- Safina (Mke, 13)
- Shangazi Lily (Mke, 33)

**SCENE THREE: CITY STADIUM PRESS CONFERENCE**

- Jonathan (Mume, 15)
- Metogba (Mume, 28)
- Komora (Mume, 14)
- Mwanaspoti na msoma habari wa runiga (Mke, 25)
- Wakasa (mwenyekiti msimamizi wa soka, mume, 54)

**SCENE FOUR: CITY STADIUM SOCCER CLINIC**

- Inspekta Tino (Mume, 40 )
- Chedede (Mume, 14)
- Safina (Mke, 13)
- Metogba (Mume, 28)
- Sauti mchanganyiko za wasichana na wavulana (13+)

**INTRO:**

**1. NARRATOR:** Nawasalimu nyote, na karibuni katika kipindi chetu cha " "Noa bongo, jenga maisha yako". Katika kipindi kilichopita, urafiki wa Chedede na Komora ulikamuliwa ndimu wakati Komora alipomsaliti Chedede kwa kuhudhuria kiliniki ya soka bila kumuarifu rafikiye. Mheshimiwa Makemba, ana mipango gani ?, na Metogba, mcheza soka mashuhuri wa kimataifa anayeongoza kliniki hiyo ya soka, anaomba fursa nyengine na wanahabari. Mwisho, shangazi lily anapoteza fahamu akiwa mbele ya Safina na Chedede. Tumeanza kuona ya kuwa, kabumbu sio mchezo tu watu uwanjani. Kaa makini na redio yako na usikilize ngano yetu leo itatufikisha wapi. Na tunafungua ukumbi, katika mkutano baina ya watu wawili wenye maisha tofauti kabisa.

**SCENE ONE : TAMBARARE CITY,CENTRAL BUSINESS DISTRICT**

2. **SFX: STREET NOISES,CAR PARKING, AUTOMATIC CAR WINDOW OPENING**

3. **MHE. MAKEMBA: (Akiita kwa sauti )** Wewe !..ndiyo,wewe kijana. Wewe ndiye Komora?

4. **KOMORA: (Scared)** Mimi? Aah hapana, lakini naweza kumtafuta.

5. **MHE.MAKEMBA:** Usinifanye mimi mjinga! Najua wewe ndiye Komora. Ungependa kutengeza hela za upesi au la?

6. **KOMORA:** Pesa? ndio, bila shaka! Lakini unataka nikufanyie nini.. Bwana….. Ee..ee..?

**7.** **MHE. MAKEMBA:** Haraka ingia garini. Lakini kwanza jisafishe kidogo.

**8.** **SFX: SOUND OF BRUSHING CLOTHES OFF WITH HANDS. CAR DOOR SHUTS, WINDOW CLOSES. CAR DRIVES OFF.**

9. **NARRATOR:** Mhe. Makemba anahitaji kitu gani kutoka kwa chokoraa kama Komora? Usishangae msikilizaji lakini ,watu wenye kutaka makubwa watafanya kila wawezalo ili lengo lao litimie. Siku ya pili Safina alirauka mapema, akafanya kazi zote za nyumbani ili awahi katika kiliniki ya soka. Swali ni, atawahi kweli?

**<u>SCENE TWO: AUNT LILY WAKES UP</u>**

10. **SAFINA: (Whispers)** Shangazi Lily... Lily... Kiamsha kinywa kitayari... Nimeshasafisha nyumba, nimeosha vyombo na kila kitu kikosafi. Tutaonana baadaye.

11. **SHANGAZI LILY: (Sleepy voice)** Hebu subiri kidogo! Una maana gani tutaonana baadaye?... ah! Kichwa changu kinauma! Ni kama niliyegongwa na basi la abiria!

12. **SAFINA:** Nafikiri ulikunywa kupita kiasi jana... ilitubidi sisi tukubebe kiti-kiti na....

13. **SHANGAZI LILY:** ? **(Alert)** Eti sisi ?. Sisi kina nani? Safina... ole wangu! Nani aliyelivunja dirisha langu? Na wewe ulikuwa wapi? Kuna chochote kilichoibiwa?

14. **SAFINA:** Kila kitu kiko Shangazi. Kuhusu dirisha, nilitaka nikueleze kabla sijaondoka. Jana kabla ya… hmm… tuyawache hayo…. kijana fulani alilivunja - na ni yeye aliyenisaidia kukuingiza ndani.

15. **SHANGAZI LILY: (Shocked)** Mamangu mzazi! Sasa nakumbuka!... Safina ushaanza kuniletea wavulana humu nyumbani mwangu?

16. **SAFINA:** Hasha! Kamwe sivyo! Dede ni rafiki yangu na tunafahamiana tu…

17. **SHANGAZI LILY:** Umesemaje ?

18. **SAFINA:**Chedede, yule kijana anayeranda randa mtaani ndiye alivunja dirisha, baadaye tukacheza kupigiana penalti, na alafu...

19. **SHANGAZI LILY: (Furious)** Chedede! Chokoraa! Ulimleta chokoraa nyumbani kwangu? Mungu wangu! kisha ukacheza kandanda!?

20. **SAFINA:** Lakini ni kijana mzuri, na alisema anakufahamu kwa kuwa umekuwa mkarimu kwake siku nyingi.

21. **SHANGAZI LILY: (Catching her breath)**Nje! Kusanya virago vyako na nyumba yangu uione paa na moshi! Nje! Toka sasa hivi!

22. **SAFINA:** Lakini, nimekosa nini shangazi Lily… **(Breaking into tears)**

23. **SHANGAZI LILY:** Umenikosea, umeniaibisha na kujiletea

yote haya. Kwanini hukufuata amri zangu? Sasa ondoka!

24. **SAFINA: (Crying)** nitakwenda wapi shangazi Lily? Sina nimjuae hapa.

25. **SHANGAZI LILY:** Hiyo ni shauri yako!

**26. SFX: BOLTS AND LOCKS BEING LOCKED.**

27. **SAFINA: (From outside)** Nisamehe shangazi Lily..tafadhali nisamehe...

28. **SFX: KNOCK ON DOOR**

29. **NARRATOR:** Maskini Safina aliachwa ameduwaa akiwa hana lolote ila mkoba tu mikononi mwake. Atakwenda wapi? Je atarudi kijijini kwa wazazi wake? Au kwa Dede? Au ataendelea kuwa na hamu ya kuhuduria kiliniki ya kabumbu? Ataepuka vipi hatari za jiji la Tambarare? Haya ndio maswali yaliokuwa akilini mwake. Wakati huohuo, Metogba alikuwa tayari katika uwanja wa michezo na Bwana Wakasa, mwenyekiti wa shirikisho la soka, wakijiandaa kuhutubia waandishi wa habari ikiwa ni siku ya pili ya kiliniki.

**SCENE THREE: CITY STADIUM PRESS CONFERENCE**

30. **METOGBA:** Siamini! Yaani watu wa nchi hii hawajui kufika katika muda unaotakiwa au nini? Mbona kila wakati wanachelewa .… Bwana mmmm.......... mwenyekiti Wakasa?

31. **WAKASA:** Unajuwa, Metogba, watu huku ni masikini hohehahe na wengi hutegemea usafiri wa umma au watembee kwa miguu...

32. **METOGBA: (cuts him short)** Mimi pia sikuzaliwa tajiri, lakini nilifunzwa umuhimu wa kuuzingatia muda. Tunapoteza muda mwingi ambao ungetumika kufanyia shughuli muhimu. Hata waandishi wa habari pia wanashindwa kulizingatia hilo?

33. **WAKASA:** Bado sijaelewa ni kwanini uliitisha mkutano mwengine na waandishi wa habari. Watu watafikiri una malengo ya kisiasa... **(Giggles)** ah.. ndiye yule pale....

34. **MWANDISHI WA MICHEZO :** Hajambo jamani... tunaweza kuanza?

35. **METOGBA:** Wako wapi wanasa vipindi vya runinga, wapiga picha na wengineo? Uko peke yako kwani?

36. **MWANDISHI WA MICHEZO:** Sijui... inaonekana umekanyaga pabaya... ukiwa tayari nitakiwasha kinasa sauti ...

37. **METOGBA: (Bluntly)** Niko tayari....

38. **SFX: TAPE RECORDER RUNNING**

39. **MWANDISHI WA MICHEZO:** Tuko hapa katika uwanja wa jiji kunakoendelea maandalizi ya timu ya vijana. Metogba, mmoja wa wachezaji maarufu na mahiri katika soka Afrika, yupo hapa tena kutupa mengi kuhusu mazoezi yao. Metgoba, mambo yanaendeleaje na vijana wetu chipukizi ?

40. **METOGBA:** Nimeita mkutano huu kwa sababu moja tu. Kuwasilisha ombi moja... Nawatolea wito raia wa nchi hii, wanasiasa, wafanyi biashara, viongozi wa kidini,waasi na makamanda wao maafisa wa serikali na mashabiki wa kabumbu. Nawaombeni tuwape nafasi watoto wetu kutimiza ndoto zao. Nisingelikuwa hapa kama sikupata nafasi ya kucheza mpira wa miguu. Kwa hivyo popote ulipo ukiusikia ujumbe huu kwenye redio, nawaomba wale walio na vijana hawa wanaowatumia kama kama wanajeshi, wakulima, wachuuzi... tafadhali wapelekeni shuleni, na wale wanaotaka kucheza soka waleteni katika kiliniki hii... asanteni sana.

41. **MWANDISHI WA MICHEZO:** Natumai mumelisikia ombi la Metogba. Labda kuna kijana angelipenda kuhudhuria kiliniki hii, anajiuliza atafaidika vipi.

42. **METOGBA:** Manufaa ni mengi. Hatujifunzi ustadi wa kandanda pekee hapa. Fauka ya hilo tutajifunza mambo kadhaa yanayohusu maisha yetu ya kila siku. Utajifunza

kuhusu ushirikiano na insi ya kuishi katika jamii. Mchezaji bora katika kiliniki hii atapewa mkataba na kilabu changu cha Ulaya atakapotimia miaka kumi na nane.Nawakumbusha kuwa timu nitakayoiteua itasafiri hadi Ulaya kushiriki katika mechi nyengine za kirafiki na hatujui ni nani atakuwa anatama mechi!.

**43.** **MWANDISHI WA MICHEZO:** Natumai mumemsikia mwenyewe Metogba! Mimi ni Lucy Lwanda kutoka Channel one.

**44.** **SFX: TAPE RECORDER STOPPED.**

45. **MWANDISHI WA MICHEZO :** Hizo ni kauli za kijasiri Metogba, nakutakia kila la heri. Sasa, mbali na hayo, ningekuomba ujihadhari na ushughulike na soka na kliniki pekee. Pindi utakapotimiza lengo shughu ushike hamsini zako. Kwa heri na kila la kheri.

46. **METOGBA:** Asante. Sasa wachezaji, munayajua mazoezi.. zungukeni kiwanja mara Tano kisha tukutane katikati. Chedede na Safina wako wapi? Komora unajua waliko?

47. **KOMORA:** Hata sina habari walipo.

48. **JONATHAN :** Kwa hivyo tufanyeje sasa? Bila wao timu haijakamilika...

49. **METOGBA:** Usitie shaka kwa sasa, Jonathan. Haya twendeni kazi !

**50.** **SFX: WHISTLE BLOWS.**

**NARRATOR:** Timu ilikuwa imevunjwa moyo na Metogba alilihisi hilo. Yeye mwenyewe alikuwa ashaanza kuwa na mitazamo tofauti kwa na hisia kuwa kuna njama inayoendelea. Jee, ataendelea au atavunjika moyo? Alipokuwa akiyawazia hayo, Dede na safina walikuwa wanaingia uwanjani. Safina amebeba mkoba wake.

**SCENE FOUR: CITY STADIUM SOCCER CLINIC**

51. **SAFINA:** Sijui nitamweleza vipi Metogba. Tumejuana naye siku moja tu.

52. **CHEDEDE:** Usiwe na wasiwasi. Niachie mimi.

53. **SFX: WHISTLE BLOWS...VOICES OF MIXED BOYS AND GIRLS**

54. **METOGBA: (Annoyed)** Sijui munanielewa vipi... lakini huko si kukimbia! Dede na Safina, nitaongea nanyi baada ya mazoezi. Ketini chini nyote. Niambieni, nguzo za timu iliyo imara ni zipi?

55. **JONATHAN:** Pesa. Ukiwa na pesa utamuajiri mchezaji unayemtaka...

56. **METOGBA:** Hapana, Jonathan. Ni kweli pesa ni muhimu na zina mchango mkubwa katika soka ya kitaalam, ila si kweli kuwa wachezaji walinaolipwa pesa nyingi ndio watakaoshinda kila wakati...

57. **CHEDEDE:** Timu nzuri ni ile yenye wachezaji wazuri wa ulinzi na mashambulizi.

58. **METOGBA:** Swadakta! Leo tutajifunza mambo hayo mawili. Kumbukeni ushirikiano ndio nguzo ya timu yoyote ya soka; walinda lango sharti washirikiane na kiungo cha kati, wao nao na washambulizi na kadhalika. Sawa, sasa...

**59. SFX: POLICE SIRENS RINGING COMING CLOSE WITH SOUND OF CAR**

60. **SFX: PLAYERS 13+ ARE IN SCHOCK, MURMURING**

61. **METOGBA:** Lahaula! Kuna nini saa? Hivi ntashatakiwa kwa kuongoza maandamano katika kliniki ya soka?

**62. SFX: SIRENS AND CAR STOPP, CAR DOOR BEING OPENED**

63. **INSPEKTA TINO:** Nani kati yenu ni Chedede?

64. **METOGBA:** Kuna shida gani afande?

65. **CHEDEDE:** Mimi ndiye Chedede.

66. **INSPEKTA TINO:** Twende! Wewe ni mtuhumiwa wa uvunjaji na wizi wa duka la Shah electronic.

67. **CHEDEDE: (Utterly shocked)** Nini, eti mimi?

**OUTRO:**

**67. NARRATOR:** Dede hakuwa pekee aliyeshangazwa na tukio hilo, Metogba na timu nzima kwa jumla walijiuliza masuali mengi. Jee tuhuma hizo ni za kweli? Mambo yatakuaje sasa… kwani Safina na timu nzima ilikuwa inamuamini Dede? Maswali ni mengi... na majibu, yako katika kipindi kijacho kwenye mchezo wetu unaoitwa "**Kabumbu barani Afrika - ni zaidi ya mchezo!".** Ukitaka kusikiliza hiki kipindi tena au kipindi chochote kilichopita, tazama kurasa za tovuti zetu katika **www.dw-world.de/lbe.** Mpaka hapo tumefikia tamati. Hadi wakati mwengine, kwa herini!